# Bongo Fleva na Siasa: Uchambuzi wa *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee* za Profesa Jay

*J. Bulaya*

**Ikisiri**

Jamii inahitaji kupatiwa elimu sahihi kuhusu siasa na masuala mengine muhimu yanayoikabili. Elimu hii inaweza kupatikana kupitia katika mfumo rasmi wa elimu, vyombo vya habari au kupitia kazi za kifasihi. Makala haya yanakusudia kuchunguza nafasi ya Bongo Fleva katika kuelimisha jamii kuhusu haki na wajibu wake pamoja na changamoto mbalimbali za kisiasa zinazowakabili wapiga kura kabla na baada ya kuwachagua viongozi wao. Katika kufikia lengo hili, makala haya yatatumia nyimbo mbili za msanii Joseph Haule (Profesa Jay) za *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee/Kikao cha Dharura*. Ili kupata hazina ya elimu iliyomo ndani ya nyimbo hizi na za wasanii wengine, makala yanapendekeza tafiti zaidi zifanyike kuhusiana na nyimbo hizi.

## 1.0 Utangulizi

Bongo Fleva ni muziki unaojadili matatizo ya kiuchumi, kisiasa, kijamii na kiutamaduni yanayoikabili jamii. Ni muziki ambao aghalabu hutoa ujumbe unaoelezea ukweli unaojitokeza katika jamii moja kwa moja na kwa uwazi. Muziki huu unaelezea matatizo ambayo hayajadiliki kwa urahisi katika jamii kupitia aina nyingine ya muziki. Bongo Fleva ni muziki unaopendwa na vijana na ambao huutumia katika kuelezea matatizo yao. Maelezo haya yanafafanuliwa na Omari (2008:73) anaposema, "…vijana wengi wa Kitanzania pia hutumia muziki huu kuelezea matatizo yao ya kila siku kama: ukosefu wa ajira na athari zake, dola na nguvu zake, umaskini na kadhalika". Omari (2008) anadai kuwa muziki huu umeshika kasi sana nchini Tanzania katika miaka ya 1990 hadi sasa. Muziki huu unazo sifa kadhaa ambazo zimeainishwa na Majembe (1998), Chachage (2002), na Omari (2008, 2009). Sifa hizo ni pamoja na matumizi ya lugha mseto na hasa kuchanganya lugha ya Kiswahili na Kiingereza, kuimba kunakoenda sambamba na matendo ya mwili, yaani matumizi ya viungo vya mwili katika utendaji wake, na sifa nyingine ni kuchanganya tamaduni. Hili linajitokeza hasa katika uvaaji na mwonekano. Wasanii wa muziki huu hupendelea kuvaa suruali na mashati makubwa, viatu vikubwa, hereni na kusuka nywele. Sifa nyingine ni matumizi ya majigambo; wasanii hutumia muziki huu kujisifia juu ya kupendwa na wanawake wengi, kipaji cha hali ya juu cha kuimba, na kupendwa na mashabiki. Sifa hizi zimeainishwa ili zitusaidie kuufahamu vizuri muziki huu, lakini hazitajadiliwa kwa kina katika makala haya.

Makala haya yanakusudia kujadili nafasi ya Bongo Fleva katika kuelimisha jamii kuhusu haki na wajibu wake. Ni makala yanayochunguza changamoto

mbalimbali za kisiasa wanazokabiliana nazo wapiga kura kabla na baada ya kuwachagua viongozi wao. Makala haya pia yanajadili wajibu walionao vingozi kwa raia. Katika kufikia lengo hili tutatumia nyimbo mbili za msanii Joseph Haule (Profesa Jay) za *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee/Kikao cha Dharura* kama zilivyonukuliwa na Omari (2009). Kupitia nyimbo hizi tutaweza kuona namna msanii anavyobainisha matatizo ya rushwa, udanganyifu, ukosefu wa elimu ya uraia, kutokuwajibika na athari zake kwa jamii.

*Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee/ Kikao cha Dharura* ni nyimbo zinazojadili masuala yanayojitokeza wakati wa kampeni za kisiasa na baada ya viongozi kuchaguliwa. Katika nyimbo hizi msanii Prosesa Jay anatoa picha inayoonesha jinsi raia, na hasa wapiga kura, wanavyopoteza haki yao na kushindwa kutimiza wajibu wao kutokana na kuhadaiwa kwa ahadi lukuki na zisizotekelezeka kutoka kwa wagombea. Katika wimbo wa *Ndiyo Mzee* msanii anaonesha ahadi zinazotolewa kwa walimu, wauguzi, wanafunzi, polisi na wakulima. Ahadi ambazo zinaonesha kuleta mabadiliko makubwa kwa raia na kuwaondolea kero mbalimbali za maisha. Msanii anajaribu kuweka wazi nguvu ya ushawishi waliyonayo viongozi wakati wa kuomba kura kwa wananchi, nguvu ambayo inachochewa na elimu ndogo ya uraia waliyonayo wapiga kura. Katika wimbo wa *Siyo Mzee/ Kikao cha Dharura*, ambao ni namba mbili, msanii anajaribu kuonesha wasiwasi wa wapiga kura kutokana na kushindwa kutekelezwa kwa yale waliyoahidiwa. Hapa msanii anaonesha mwamko wa wananchi wa kuthubutu kuhoji juu ya ahadi walizoahidiwa. Katika wimbo huu msanii anaonesha jinsi wapiga kura wasivyokubaliana na majibu yanayotolewa jukwaani na kiongozi wao. Mwishoni mwa wimbo huu kikao kinaisha bila maafikiano kati ya kiongozi na wapiga kura, hali inayosababisha kuomba msaada kutoka kwa polisi kwa lengo la kutuliza ghasia. Msanii wa wimbo huu anakusudia kuonesha jinsi wananchi walivyochoshwa na hali ngumu ya maisha pamoja na kutokuona mabadiliko waliyoyategemea kutoka kwa kiongozi wao.

## 2.0 Dhamira katika *Ndiyo Mzee* na *Siyo Mzee/Kikao cha Dharura*

Sehemu hii tunakusudia kujadili dhamira zinazoshughulikiwa na msanii katika nyimbo zilizotajwa hapo juu. Kupitia nyimbo hizi msanii amejaribu kutoa ujumbe wenye lengo la kuielimisha jamii juu ya changamoto mbalimbali za kisiasa zinazoikabili jamii ya Kitanzania. Changamoto zinazoibuliwa na msanii katika nyimbo hizi zinatoa mwanya kwa viongozi kutafakari kwa makini juu ya kiwango cha elimu ya uraia waliyonayo wananchi, rushwa wakati wa kampeni, udanganyifu na ahadi hewa zinazotolewa wakati wa kampeni, kutokuwajibika, na kuwataka wanajamii kutafuta njia ya kukabiliana na hali hiyo.

Tukianza na wimbo *wa Ndiyo Mzee*, kwanza msanii anaonesha ahadi hewa zisizotekelezeka zinazotolewa na wagombea wakati wa kuomba nafasi mbalimbali za uongozi. Katika mistari ifuatayo msanii anabainisha matatizo mbalimbali yanayozikabili asasi na taasisi mbalimbali za serikali na zisizo za kiserikali ambayo mgombea anayatumia kama njia ya kujipatia kura kutoka kwa wananchi, huku akiwapa matumaini kuwa akiingia madarakani kila kitu kitawezekana. Kwa mfano msanii anasema:

> Ni mambo madogo tu, nadhani nitarekebisha
> Mkinipa visiku vichache tu uchumi utapanda ile ghafla bin vu
> Nataka mpaka Matonya afundishe Chuo Kikuu
> Nchi ya Tanzania itang'aa ile kishenzi
> Na nitahakikisha kila barmaid anamiliki benzi
> Wanafunzi mkafanyie practical mwezini
> Kwenye hospitali nitamwaga dawa kama mchanga
> Na nitafungua akaunti kwa kila mtoto mchanga
> Mabomba yatatoa maji na maziwa kwa nchi nzima
> Mkulima kila mmoja nitampatia trekta...

Msanii katika mistari hii anasawiri hali halisi ya jamii ambayo wagombea wake wa uongozi wanayatumia matatizo ya wananchi kama mtaji wa kupata madaraka. Miongoni mwa matatizo ambayo yametajwa ni pamoja na mazingira duni ya kazi, mazingira duni ya elimu, huduma hafifu za afya na hasa upatikanaji wa dawa, huduma za maji na matatizo ya wakulima hasa upatikanaji wa pembejeo. Kutokana na matatizo haya wananchi wanashawishika kumchagua mgombea kwa matumaini ya kupata utatuzi wa matatizo yao ndani ya muda mfupi tu.

Pili, katika wimbo huu msanii anatumia kibwagizo cha *Ndiyo Mzee* kuukejeli mfumo mzima wa utoaji wa elimu ya uraia kwa wananchi, mfumo ambao umewaacha wananchi katika ujinga na kutokujua haki na wajibu wao katika siasa na mambo mengine yanayowahusu katika jamii. Ni kibwagizo kinachowakejeli wananchi ambao mara zote hukubali pasipo kuchuja ujumbe au ahadi zinazotolewa na viongozi wao. Raia wanaoamini maneno pasipo kupima uwezekano wa kutimizwa kwa ahadi wanazoahidiwa. Vilevile, msanii anatumia kibwagizo hiki kuwakejeli viongozi ambao wanaamini kuwa madaraka hupatikana kwa ahadi na uongo mwingi. Viongozi wanaotoa ahadi bila kupima uwezekano wa kutekelezeka kwake. Turejee katika kibwagizo kifuatachao:

| | |
|---|---|
| Si mtafurahi Watanzania jamani? | Ndiyo mzee! |
| Si kweli nakubalika jamani? | Ndiyo mzee! |
| Basi mimi ni mkombozi wenu jama? | Ndiyo mzee! |
| Na nitafuta shida zenu zote. | Ndiyo mzee! |
| Hivi ni nani ni vijimambo tu. | Ndiyo mzee! |
| Na hatamu tutaishika ok? | Ndiyo mzee! |

Tatu, katika wimbo huu msanii anaweka wazi matatizo ya ushirikina na matumizi ya vyeti bandia, na athari zake kwa jamii. Katika kufikisha ujumbe wake kwa jamii, mwandishi anaonesha jinsi vitendo vya ushirikina vinavyojitokeza wakati wa kupiga kampeni. Msanii anamuonesha mgombea akiwa kwa 'Kalumanzila' yaani mganga wa kienyeji ili kusaidiwa kushinda katika uongozi. Hali hii inaakisi hali halisi ya jamii, kwani kwa kiasi kikubwa inahusishwa na vitendo vya kikatili au mauaji ya vikongwe na maalbino katika jamii, vitendo vinavyochochewa na kutafuta madaraka miongoni mwa wagombea au kutafuta utajiri. Kwa mfano, mwandishi anasema:

Tumemfuma wenyewe kwa Kalumanzila anasafishwa
Kalumanzila akamwambia 'eee shida yako?'
'Eleza faster faster kabla jini hajapanda'

Msanii wa wimbo huu pia anagusia suala la taaluma na matumizi ya vyeti vya bandia kwa wagombea ili kujipatia nafasi za uongozi. Suala hili linajitokeza katika jamii na kuathiri sekta za elimu, afya, na sekta nyingine za jamii katika utendaji na maamuzi kwa kukosa watu wenye taaluma na ujuzi wa kweli. Katika wimbo huu msanii anatilia mashaka uwezo wa kitaaluma wa mgombea wake. Rejea mistari hii msanii anaposema:

Sio mzuri ni muongo tu mnafiki
Na ni kiburi kimsuli anaongopea sana
Amepita pita school lakini mambo yake si mazuri
Wala tusimtegemee atatuangamiza

Pamoja na wapiga kura kupewa tahadhari dhidi ya tabia, elimu na uwezo alionao mgombea katika kuongoza, wananchi wanaamua kumchagua kuwa kiongozi wao. Hali hii inatokana na kukosekana kwa elimu ya uraia inayompa mpiga kura urazini na uwezo wa kuamua kuchagua kiongozi pasipo kuhadaiwa na sifa lukuki wanazojipachika wagombea. Hali hii haiwezi kuisha pasipo jitihada za makusudi kuchukuliwa, hatua za kuwapatia wapiga kura elimu ya uraia itakayowawezesha kujua na kutimiza wajibu wao kama wananchi.

Katika wimbo wa *Siyo Mzee/Kikao cha Dharura*, mwandishi anaweka wazi majibu ya kutoridhisha yanayotolewa na viongozi baada ya kushindwa kutimiza ahadi walizotoa. Anaonesha namna viongozi wanavyokwepa lawama na

kujitetea kwa kila namna baada ya kushindwa kutekeleza wajibu wao. Msanii pia anaonesha namna viongozi wanavyokerwa na maswali yanayotaka kujua ukweli au kutimizwa kwa ahadi walizozitoa. Katika wimbo huu msanii anawavisha wahusika wake ujasiri na hali ya kujiamini katika kuuliza maswali yanayohusu maslahi yao. Hii ni tabia ya kuigwa na wananchi; msanii anawahamasisha wananchi kudai haki zao pasipo uoga. Maswali yanayoulizwa katika wimbo huu yanahusu sekta za ulinzi, kilimo, miundombinu, maji na uchumi. Msanii amejitahidi kwa kiasi kikubwa kuonesha matatizo yanayowagusa wananchi moja kwa moja. Katika kufafanua haya msanii anasema:

> Naitwa sajenti Bwemero kwa niaba ya jeshi la polisi
> Nilikuwa nauliza zile helkopta zetu vipi?
> Mheshimiwa sisi wakulima ulituahidi matrekta
> Na siku zinayoyoma tu mbona hatujaletewa?
> Ulituahidi utatujengea barabara tano chini na juu...
> Umeyafumbia macho mheshimiwa huoni haya?
> Eeh vipi mabomba kutoa maji na maziwa nchi nzima?
> Mzee hali ni mbaya si tutagawana vya kwako?

Katika wimbo huu msanii anamtumia kiongozi au mgombea kuwakilisha tabaka la viongozi lisilokuwa na nidhamu kwa wananchi waliowaweka madarakani. Mwandishi anaonesha hali ya wazi ya kulewa madaraka na kiburi. Tabia hii inajidhiirisha katika majibu ambayo kiongozi anayatoa kwa wananchi. Katika msitari wa 1 hapo chini kiongozi anawataka wananchi waulize maswali ya kiutu uzima. Hapa tunajiuliza, maswali ya kiutu uzima ni yapi? Na ni kwa maslahi ya nani? Na katika mstari wa 2 msanii anaonesha jinsi kiongozi anavyokuwa kigeugeu kwa kukana ahadi alizozitoa. Ni wazi kuwa viongozi wa namna hii hawapaswi kupewa nafasi yoyote ya uongozi katika jamii. Ili kudhihirisha haya msanii anasema:

> Jamani naomba muulize maswali ya kiutu uzima.
> Mlininukuu vibaya nasisitiza haiwezekani.

Katika wimbo huu msanii anawakejeli viongozi wasiopenda kuachia madaraka hata kama katika muda wao hawakufanya vizuri. Msanii katika wimbo huu anaonesha namna mgombea anavyoshindwa kuachia madaraka baada ya kushindwa kutimiza ahadi alizotoa kwa wapiga kura wake, badala yake anaendelea kutoa ahadi na kuahidi kufanya vizuri akipata nafasi nyingine tena. Miongoni mwa sababu anazozitoa ni pamoja na kukosa muda wa kutosha kufanya yale yote aliyowaahidi na hivyo akiongezewa muda atafanya vizuri zaidi. Katika kuthibitisha hili msanii anasema:

> Mkinichagua tena mtakwenda huko mapema
> Na nitatekeleza kila neno ninalosema

Sema nimesongwa na haka kamuda
Mkiniongeza muda kila kitu babu kubwa

Kibwagizo cha wimbo huu pia kinaonesha hali ya wananchi kutokukubaliana na majibu ya kiongozi wao. Hali hii inasababishwa na kutotimiziwa kwa ahadi walizoahidiwa. Msanii anawatumia wananchi wa kada mbalimbali kufikisha ujumbe huu kwa jamii. Katika kibwagizio hiki msanii anawataja washika dau, wapiga debe na wakulima kuwawakilisha wananchi wa kada nyingine wasioridhishwa na utendaji wa viongozi wao. Wananchi hawa wanajibu kwa pamoja, (siyo mzee) kuonesha kutokukubaliana na kiongozi wao. Msanii anawahamasisha wananchi kuwa na sauti ya pamoja katika kupinga na kukemea vitendo visivyofaa. Anawataka wanajamii wote waungane katika kuwapinga viongozi wasiotekeleza wajibu wao. Katika mistari hii hapa chini msanii anasema:

| | |
|---|---|
| Wananchi tupo pamoja hapo? | Siyo mzeeee |
| Watanzania tunaelewana kule? | Siyo mzeeee |
| Washika dau na wapiga debe hapo? | Siyo mzeeee |
| Eheeehh? | Siyo mzeeee |
| Eti? | Siyo mzeeee |
| Wakulima tupo pamoja pale? | Siyo mzeeee |
| Wananchi tunaelewana kule? | Siyo mzeeee |

Wimbo huu ni changamoto kwa serikali na asasi zinazotoa elimu ya uraia kwa lengo la kuwasaidia wananchi kutambua wajibu walionao kwa nchi yao na umuhimu wa uchaguzi wanaoufanya katika maisha yao ya kila siku na katika kuliletea taifa maendeleo. Fundisho tunalolipata hapa ni kuwa elimu ya uraia itolewe katika ngazi zote za elimu, kwa kila raia na isisubiri kutolewa wakati wa kuelekea katika chaguzi. Wakati wote wananchi waelimishwe kuhusu haki na wajibu wao kama raia. Kwa kufanya hivyo tutajenga taifa linaloheshimu, kulinda, kutetea na kutekeleza haki na wajibu wa raia wake.

Mwisho, msanii anaonesha jinsi jamii inavyopata urazini; jamii inazinduka kifikra na kuonesha kwa vitendo kuchoshwa na kiongozi wao. Hali hii inaonesha kuwa wananchi wanataka mapinduzi ya kweli. Mapinduzi yatakayowafikisha katika uamuzi wa kweli. Hii ni changamoto kwa jamii ya Kitanzania, Kiafrika na Ulimwengu kwa ujumla. Msanii anatukumbusha kuwa ni wakati ambao Watanzania, Waafrika na dunia yote wanapaswa kuwakataa viongozi wasiowafaa, wasaliti, wanaotumia maneno mengi kuwarubuni ili kupigiwa kura na baada ya kupata madaraka kuwasahau. Msanii anasawiri vema hali inayojitokeza katika nchi za Ivory Coast, Misri, Yemen na Tunisia, nchi ambazo wananchi kwa pamoja wameamua kuandamana na kuupinga uongozi dhalimu usiotetea maslahi yao. Mkabala ambao labda unaweza

kufuatwa na nchi nyingine kadhaa siku zijazo. Katika mistari ifuayato msanii anasema:

> Nadhani ndugu zangu tuko pamoja..... (aah wapi!)
> Jamani tupunguzeni jazba basi kidogo..... (hatutaki!)

## 3.0 Hitimisho

Makala haya yametumia nyimbo mbili tu za msanii Joseph Haule (Profesa Jay) kuonesha mchango wa Bongo Fleva katika kuelimisha jamii juu ya wajibu wake katika kuleta mabadiliko. Nyimbo hizi zimetumika kama kielezo tu, tunaweza kutumia nyimbo za wasanii wengine na kuona jinsi wanavyosawiri hali ya jamii. Kwa mfano, tunaweza kuchunguza na kuona jinsi wanamuziki wa Bongo Fleva wanavyolitazama suala la UKIMWI na magonjwa mengine ya ngono, utoaji wa huduma za jamii kama elimu, haki na afya, mimba katika umri mdogo, na suala la mapenzi. Hoja hii pia inaungwa mkono na Senkoro (2003), anapobainisha kuwa wanamuziki wa muziki huu, hutumiwa kama njia ya kuelezea matumaini, masononeko, kukata tamaa na matarajia yao. Kwa hiyo kwa kuhakiki na kuchunguza nyimbo hizi, jamii itanufaika na mafunzo au ujumbe unaobebwa ndani yake.

## Marejeleo

Chachage, C.S.L. (2002). "Ndani ya Bongo: Utandawazi na Migogoro ya Utamaduni." Makala Iliyowasilishwa katika Mkutano wa Kumi wa Hali ya Siasa Tanzania. Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Majembe, A.K. (1998). "Language Use in Tanzania's Hip hop Scene." Unpublished Research Paper. University of Dar es Salaam.

Omari, S. (2008). "Mitindo na Matumizi ya Lugha katika Muziki wa Kizazi Kipya Tanzania."katika Jarida la Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Juzuu 69 uk 73-92.

Omari, S. (2009). 'Tanzania Hip hop Poetry as Popular Literature', Unpublished PhD Thesis, University of Dar es Salaam.

Senkoro, F.E.M.K. (2003). "Rethinking Popular Arts and Culture in the 21th Century East Africa." Makala Iliyowasilishwa katika Maadhimisho ya 30 ya CODESRIA.

**Diskografia**

Profesa Jay. (2003). *Mapinduzi Halisi*, Dar es Salaam: GMC Wasanii Promoters.

## Kiambatisho 1: *Ndiyo Mzee*

**Utambulisho**

1. Naam ndugu wananchi
2. MC wenu babu Ayubu ninawaleteeni habari
3. Kuhusiana na huyu mgombea wetu, bwana
Joseph Haule,
4. Mpe kura za ndiyo kwa kuwa yeye ni mpenda watu
5. Ni mpenda amani na ni mtu mwenye huruma kwa watu wote
6. Kwa hiyo basi nawaomba ndugu wananchi mumpe kura ya ndiyo (makofi)
7. Naam basi, hivyo basi ndugu wananchi eeh tafadhari
8. Namkaribisha mgombea wetu bwana Joseph Haule ili aje kuzungumza na wananchi. Karibu

**Ubeti 1**

9. Ok ok naitwa Joseph Haule mwana wa Msolopogazi
10. Nadhani nimeletwa kuokoa hiki kizazi
11. Mimi ni mwanasiasa niliyabarikiwa na Mungu
12. Nimeletwa kwenu waungwana niwapunguzie machungu
13. Mimi ni mteule Kusini mwa Jangwa la Sahara
14. Ndiyo maana nimetunukiwa cheti cha juu cha utawala
15. N'na hekima kuliko mfalme Suleimani msiwe na wasawasi
16. Na hii nitadhihirisha pindi mtakaponipa nafasi
17. Actually, nimedhamiria kuwasaidia
18. Taifa lenye nguvu duniani liwe Tanzania
19. Jamani makofi tafadhari basi jamani (makofi)
20. Ni mambo madogo tu, nadhani nitarekebisha mkinipa visiku vichache tu uchumi utapanda ile ghafla bin vu
21. Nataka mpaka Matonya afundishe Chuo Kikuu
22. Nchi ya Tanzania itang'ara ile kishenzi
23. Na nitahakikisha kila barmaid anamiliki benzi
24. Si mtafurahi dada zangu jamani? Ndiyo!

**Ubeti II**

44. Wafanyakazi wa serikalini nashangaa hamna magari
45. Yaani hata mikweche, ha! ha! Hii ni hatari
46. Na nina mpango wa kuongeza mishahara iliyo minono
47. Mara mia moja ya ile ya mwanzo iliyofanya mfanye migomo
48. Nitawapa nyumba nzuri na majumba ya kifahari
49. Watu watashangaa mtakapopita kila mahali
50. Mkulima kila mmoja nitampatia trekta
51. Nadhani hiyo ndiyo itasaidia kunyanyua sekta
52. Mtauza nafaka zenu bilioni kwa mabilioni
53. Watu midomo wazi kama wameshika ugoni
54. Walimu zawadi zenu mh nimezificha moyoni
55. Nadhani mtazimia siku mkizitia machoni.
56. We acha tu, mtafurahi ninyi
57. Ila hapa hapamfai mtu mwingine niwekeni mimi
58. By the way polisi wote mi nawasifu
59. Jinsi mnavyokwenda sahani moja na wahalifu
60. Sasa kila mmoja nitampatia helkopta
61. Nadhani hiyo ndoto wote hamjawahi kuota
62. Raia wa Tanzania mtalala mlango wazi
63. In fact n'na uhakika wa kudhibiti ujambazi
64. Nitajenga barabara tano tano chini na juu
65. Nitajenga kumbi nyingi sana za starehe baharini
66. Napendwa kuitwa mshumaa kumulikia wenzangu
67. Na mtakaoyumba kiuchumi tutagawana vya kwangu

**Rudia Kiitikio**

**Ubeti III: Babu Ayubu**

68. Ndugu wagombea kuna mtu ana swali kutoka kwa
Mgombea?
69. Nauliza hivi kuna mtu ana swali kutoka kwa mgombea?
70. Basi ajitokeze ili aweze kuuliza swali

**Mpiga Kura**

71. Nyie ndugu huyu msimpe kura
72. Sio mzuri mwongo tu mnafiki na ni kiburi kimsuli
73. Anaongopea sana sijui kazaliwa muda gani
74. Asubuhi au alasiri?
75. Au wakati wa mvua zile za kipindi kile

25. Basi endeleeni kunisifu kwa nyimbo na mapambio
26. Nipeni hiyo nafasi jamani hamuoni hali ni mbaya?
27. Nataka kuigeuza Tanzania kama Ulaya
28. Cha kwanza nitakachokifanya nitafuta umaskini
29. Wanafunzi mkafanyie practical mwezini
30. Kwenye mahospitali nitamwaga dawa kama mchanga
31. Na nitafungua akaunti kwa kila mtoto mchanga
32. Mabomba yatatoa maji na maziwa nchi nzima
33. Watu wa vijijini mtasahau habari ya visima
34. Nitafadhiri wachawi waweze kutengeneza ndege
35. Kila mtu awe na yake makonda na wapiga debe

**Kiitikio**

36. *Si mtafurahi Watanzania jamani? Ndiyo mzee*
37. *Sikweli nakubalika jamani? Ndiyo mzee*
38. *Basi mimi ni mkombozi wenu jama? Ndiyo mzee*
39. *Na nitafuta shida zenu zote Ndiyo mzee*
40. *Hivi ni nani ni vijimambo tu Ndiyo mzee*
41. *Na vinanikera kweli kweli mimi Ndiyo mzee*
42. *Basi hali itabadilika sawa? Ndiyo mzee*
43. *Na hatamu nitaishika ok? Ndiyo mzee*

76. Amepitapita school lakini mambo yake si mazuri
77. Wala tusimtegemee atatuangamiza
78. Labda angesubiri kwanza uchaguzi umekwisha
79. Tumemfuma wenyewe kwa Kalumanzila anasafishwa
80. Kalumanzila akamwambia 'eee shida yako?'
81. 'Eleza faster faster kabla jini hajapanda'
82. Eeh tya hajakaa vizuri mashetani si yakamuanza
83. Kakurupuka kwa kasi ya kimbunga amejichanja
84. Tulisikia akisema kwa sauti kubwa ya kukaripia
85. 'Sya waungwana munisaidie ndo nitamweleza…'
86. Uongo mtupu babake ameliwa
87. Waungwana wamempeleka chau mpaka kaibiwa
88. Yupo hamna tafu na bufi amewehuka
89. Hajatulia huyu mpepeeni uuuuh uuuuh
90. Ni sauti ilyosikika kutoka kwa mzee wa pembeni
91. Sijui msaidizi mganga au mpelelezi
92. Na kwa taarifa yako uongozi hupati ng'oo
93. Labda urudi kwenu uende ukavunje tunguli
94. Na hao waganga wako waeleze hupati kitu hapa hata utoe chapaa eeeh eeeh.

**Kiitikio**

95. *Je, wananchi mmenisikia Ndiyo Mzee!*
96. *Kuwa huyu jamaa hatufai Ndiyo mzee!*
97. *Na inafaa kumchukia Ndiyo mzee!*
98. *Hatumtaki aondoke zake Ndiyo Mzee!*
99. *Tusikubali na maneno nyake Ndiyo Mzee!*
100. *Tunahakikisha hatumchagui Ndiyo Mzee!*
101. *Kwa sababu jamaa ni mnafiki Ndiyo Mzee!*
102. *Asitufanye tuwe na dhiki Ndiyo Mzee*

## Kiambatisho 2: *Siyo Mzee/ Kikao cha Dharura*

**Ubeti I: Profesa Jay**

1. Nawashukuru sana wananchi kwa kuweza kunipa kura
2. Nashangaa nimeitwa ghafla kwenye kikao cha dharura
3. Kikao kinaashiria kina maswali juu yangu
4. Hii inatokana na Ndiyo Mzee na ahadi yangu
5. Naona watu ni wengi wananchi walio na maana
6. Najaribu kutafakari nini kinawachanganya
7. Nipo tayari kujibu maswali yenu zamu kwa zamu
8. Watakaouliza maswali na ningependa niwafahamu

**Swali**

9. Naitwa sajenti Byemero kwa niaba ya jeshi la polisi
10. Nilikuwa nauliza zile helkopta zetu vipi?

**Jibu**

11. Nafikiria kwanza kuanzisha chuo cha marubani
12. Vinginevyo mtapata ajali nyingi sana angani
13. Baiskeli hamjui kuendesha helkopta mtaendeshaje?
14. Kila mtu aendeshe yake huko angani itakuwaje?

**Swali**

15. Mheshimiwa sisi wakulima ulituahidi matrekta
16. Na siku zinayoyoma tu mbona hujatuletea?

**Jibu: Profesa Jay**

17. Wakulima mngeendelea tu kutumia jembe la mkono
18. Serikali haina hela bajeti imefika kikomo
19. Naona kilimo cha mkono kinaedelea vizuri
20. Jamani kazeni mikono endeleeni kukaza misuli

**Kiitikio**

21. Wananchi tupo pamoja hapo? (Siyo mzeeeeeee)
22. Watanzania tunaelewana kule? (Siyo mzeeeeee)
23. Washikadau na wapiga kura pale? (Siyo mzeeee)
24. Eeehh? (Siyo mzeeee) Eti? (Siyo mzeeeeeeee)
25. Wakulima tupo pamoja pale? (Siyo mzeeeee)
26. Wanafunzi tunaelewana kule? (Siyo

39. Kuhusu vibarabara naomba muondoe shaka

**Swali**

40. Eeh vipi mabomba kutoa maji na maziwa nchi nzima?

**Jibu: Profesa Jay**

41. Jamani naomba muulize maswali ya kiutu uzima
42. Mabomba kutoa maji na maziwa haiwezekani
43. Mlininukuu vibaya nasisitiza haiwezekani

**Swali**

44. Mzee hali ni mbaya si tungegawana vya kwako?
45. Kwenye kampeni zako si ilikuwa ahadi yako?

**Jibu: Profesa Jay**

46. Eeehh? Kugawana vya kwangu hilo suala litakuwa gumu
47. Familia itanitazama ebo, nina majukumu
48. Imeandikwa kila mtu atabeba msalaba wake
49. Kila mbuzi ale urefu wa kamba yake
50. Mbona mnaniuliza maswali mengi kunikomoa?
51. Jamani Watanzania tunajenga tunabomoa?

**Rudia Kiitikio**

**Ubeti III: Profesa Jay**

52. Wafanyakazi wa serikalini sasa ninyi magari ya nini?
53. Daladala chungu nzima mnaweza kuwahi kazini
54. Nasema mnapenda sana starehe kuliko kazi
55. Na hiyo ndiyo sababu mnaharibu hiki kizazi
56. Wanafunzi niliwaahidi mtafanyia practical mwezini
57. Kabla ya kuwapeleka huko mi nilifanya utafiti
58. Nimegundua huko mwezini kweli kuna baridi sana
59. Na pia kuna vitisho kuwepo kambi za Obama
60. Mkinichagua tena mtakwenda huko mapema

mzeeeee)
27. Mabaamedi na mapolisi pale? (Siyo mzeeeee)

**Ubeti II: Profesa Jay**
28. Mabaamedi ondoeni hofu kilio chenu nimekisikia
29. Mabenzi yenu yapo bandarini tayari yameshawadia
30. Nimemchagua kiranja ili anipe idadi yenu
31. Niwape funguo muondoke na magari yenu

**Swali**
32. Ulituahidi utatujengea barabara tano tano juu na chini
33. Hizo zote hatutaki tunataka moja tu ya baharini
34. Kila siku tunapita barabara zinakuwa mbaya
35. Umeyafumbia macho mheshimiwa huoni haya?

**Jibu: Profesa Jay**
36. Barabara ya Mkwekwe nimeshamwaga kifusi
37. Baada ya wiki mbili itakuwa safi kama Urusi
38. Makandarasi wanafanya kazi kutoka China Madagascar

61. Na nitatekeleza kila neno ninalosema
62. Sema nimesongwa na haka kamuda
63. Mkiniongezea muda kila kitu babu kubwa
64. Wengine kimya na maswali yamepungua
65. Yeyote mwenye swali ningependa kumtambua
66. Naona mnanong'ona wengine mmekunja sura
67. Hii inaonesha mmeridhika kunipa kura!
68. Nadhani ndugu zangu tuko pamoja... (Aah wapi!)
69. Jamani tupunguzeni jazba basi kidogo ....(Hatutaki)
70. Sasa Watanzania mbona mnaanzisha vurugu
71. Nadhani mmesahau Watanzania wote ni ndugu

**Babu Ayubu**
72. Eeeeh? Jamani nasema hivi kikao kimeahirishwa
73. Jamani maafande... Afande Miraji.... Afande Mzafalu...afande nani Gondwe njooni mtusaidie.

**Rudia Kiitikio**